TANGAZO LA SERIKALI Na. 25 la tarehe 12/1/2024

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45(2)(i))*

KANUNI ZA MATUMIZI YA MFUMO WA UFUATILIAJI MWENENDO WA VYOMBO VYA USAFIRI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

## MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

*Kanuni* *Jina*

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
IDHINI KWA WASAMBAZAJI

4. Maombi ya cheti cha idhini ya kusambaza vifaa.
5. Vigezo vya kumuidhinisha msambazaji.
6. Kufanya majaribio ya vifaa.
7. Idhini kwa msambazaji wa vifaa.
8. Cheti cha idhini.
9. Kuhuisha cheti cha idhini.
10. Kusimamisha cheti cha idhini.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI KWA MSAMBAZAJI WA VIFAA

11. Masharti kwa msambazaji wa vifaa.

12. Masharti kwa mtoa huduma.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA UJUMLA

13. Vifaa visiathiri utendaji kazi wa chombo.
14. Gharama za huduma za kadi ya simu.
15. Maombi ya upatikanaji wa VTS.
16. Makosa na adhabu.
17. Mapitio.
18. Rufaa.

MAJEDWALI

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI,
(SURA YA 413)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 45(2)(i))*

KANUNI ZA MATUMIZI YA MFUMO WA UFUATILIAJI MWENENDO WA VYOMBO VYA USAFIRI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**.Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Matumizi ya Mfumo wa Ufuatiliaji Mwenendo wa Vyombo vya Usafiri za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Kanuni hizi zitatumika kwa wasambazaji wa vifaa vya ufuatiliaji mwenendo wa vyombo vya usafirishaji pamoja na watoa huduma wa usafirishaji katika masuala ya ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo kwa Tanzania Bara.

Tafsiri

**3**. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 413

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya Sheria;

"Programu ya maombi kutambuana" kwa kifupi "API" maana yake ni namna ambayo program za kompyuta mbili tofauti au zaidi zinaweza kuwasiliana kwa pamoja;

Sura. 130

"Mamlaka ya Viwango" maana yake ni Mamlaka ya Viwango na Ubora ya Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Viwango;

"Kifaa cha Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Chombo" kwa kifupi "VTD'' maana yake ni kifaa na viunganishi vyake vinavyounganishwa kwenye chombo cha umma chenye

uwezo wa kutunza kumbukumbu na kuhamisha taarifa za muda huo kwenye mfumo;

"Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Chombo" kwa kifupi "VTS" maana yake ni mfumo unaopokea, kutunza, kufuatilia na kuonesha kwa wakati mwenendo wa chombo cha usafiri wa umma;

"Msambazaji" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa au taasisi ya serikali inayoshughulika na kusambaza na kufunga kifaa VTD;

T.S Na. 76 la 2020

"mtoa huduma" maana yake ni mtu au kampuni iliyopewa leseni kama mmiliki wa chombo cha moto chini ya Kanuni za Leseni za Usafirishaji za Magari ya Kubeba Abiria kwa kutoa huduma zinazodhibitiwa;

"Mfumo Unaotumika Duniani kwa Mawasiliano" kwa kifupi "GSM" maana yake ni mtandao unatumika na mitandao ya simu kwa kiasi kikubwa duniani kwa kuhamisha taarifa; na

"Mfumo Unaotumika Duniani kwa Urambazaji" kwa kifupi "GPS" maana yake ni mfumo wa urambazaji unaotumia satelaiti, kipokeaji na algoriti ili kusawazisha data ya eneo, kasi na wakati wa usafiri wa anga, baharini na ardhini.

## SEHEMU YA PILI
## IDHINI KWA WASAMBAZAJI

Maombi ya cheti cha idhini cha kusambaza vifaa

**4**.-(1) Mtu anayetaka kusambaza na kuweka VTD kwenye chombo cha usafirishaji anatakiwa aombe idhini kwa Mamlaka kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi na kulipa ada ya maombi iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na-

(a) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni;
(b) nakala halali ya leseni ya biashara;
(c) nakala ya hati miliki au nakala ya mkataba wa pango wa ofisi;
(d) nakala halali ya cheti cha hati safi ya mlipa kodi; na
(e) sampuli ya VTD inayotarajiwa kufungwa.

Vigezo vya kumuidhinisha msambazaji

**5**.Mamlaka inaweza kumuidhinisha msambazaji wa VTD chini ya kanuni kama-

(a) Msambazaji ni kampuni iliyosajiliwa Tanzania au Taasisi ya Serikali;

(b) Msambazaji ametoa nyaraka za kiufundi ya vifaa kwa ajili ya kuchukua kumbukumbu na kuchakata taarifa inayopelekwa;

(c) Msambazaji ana VTD ambayo-

(i) ina uwezo wa kuchukua kumbukumbu, kutunza na kuhamisha taarifa kwa muda huohuo;

(ii) ina viwango vilivyowekwa na Mamlaka ya Viwango;

(iii) haina athari katika uendeshaji wa chombo cha usafirishaji;

(iv) ina uwezo wa kuchukua kumbukumbu na kuhifadhi matukio au taarifa hata kusipokuwa na mtandao na taarifa hizo kusoma pindi mtandao utakaporudi;

(v) ina uwezo wa kutuma taarifa kwa mfumo wa Mamlaka wa ufuatiliaji mwenendo wa chombo;

(vi) ina uwezo wa kutuma alama za GPS kwa muda mahsusi;

(vii) isishindwe kufanya kazi hata pale kifaa kitakapokuwa kimechomoka kutoka kwenye umeme, umeme umekatika au pale alama ya mwendokasi au waya utakapokuwa umechomoka chombo hakitaweza kwenda kwa mwendokasi uliozidi;

(viii) ina vifaa vya kukubali kifaa cha nje na kuwezesha muunganisho wa mbali kwa ajili ya kujaribu VTD na kuthibitisha utendakazi wake;

(d) msambazaji ana wafanyakazi wenye ujuzi wa kutosha wa kuunganisha na kuhudumia kifaa cha ufuatiliaji wa mwenendo wa vyombo;

(e) msambazaji amewasilisha kwa Mamlaka Cheti cha Uthibitisho cha mtengenezaji wa VTD na uthibitisho wa waranti ya angalau mwaka mmoja kwa VTD;

(f) msambazaji amekidhi vigezo vya utekelezaji vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili baada ya majaribio chini ya Kanuni hizi; na

(g) msambazaji amelipa ada stahiki kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Majaribio ya Utendaji kazi wa VTD

**6**. Baada ya kupokea maombi, Mamlaka itamtaka Msambazaji kuwezesha kifaa kufanya kazi na kukifunga kwenye chombo kwa ajili ya majaribio.

Idhini kwa msambazaji wa VTD

**7**.-(1) Mamlaka inaweza, ndani ya siku kumi na nne kumuidhinisha Msambazaji kusambaza VTD baada ya kupokea maombi na kuridhika na vigezo vya msambazaji chini ya kanuni ya 5 na majibu ya majaribio ya utendaji kazi wa VTD kwa mujibu wa kanuni ya 6.

(2) Mamlaka inaweza kukataa kumuidhinisha msambazaji wa VTD endapo-

(a) muombaji atashindwa kukidhi vigezo vya kanuni ya 5;

(b) muombaji amejihusisha na vitendo vya kukosa uaminifu au uongo;

(c) muombaji atashindwa kulipa ada stahiki; na

(d) VTD ya muombaji itashindwa majaribio chini ya kanuni ya 6.

(3) Endapo Mamlaka itakataa kutoa idhini kwa msambazaji inaweza kumuagiza muombaji kurekebisha mapungufu yaliyobainika na kurudisha kwa Mamlaka ndani ya siku kumi na nne.

(4) Endapo muombaji atashindwa kufanya marekebisho ndani ya siku thelathini tangu kukataliwa kupewa idhini, atatakiwa kuwasilisha maombi mapya.

Cheti cha idhini

**8**.-(1) Mamlaka itatoa cheti cha idhini kwa msambazaji wa VTD aliyeidhinishwa.

(2) Cheti cha idhini kitakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitatu na kinaweza kuhuishwa.

(3) Msambazaji aliyeidhinishwa atatakiwa kulipa ada stahiki kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Kuhuisha cheti cha idhini

**9**.-(1) Mmliki wa cheti cha idhini anapaswa kuwasilisha maombi ya kuhuisha cheti ndani ya siku thelathini kabla ya cheti chake kuisha muda wake kwa kutumia fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Maombi ya kuhuisha yataambatishwa na nyaraka zifuatazo-

(a) nakala ya leseni ya biashara;
(b) nakala halali ya hati safi ya malipo ya kodi; na,
(c) nakala ya hati miliki au mkataba wa pango wa ofisi kama kuna mabadiliko.

(3) Mamlaka inaweza kuhuisha cheti cha idhini baada ya kupokea maombi ya kuhuisha chini ya Kanuni hizi.

Kusimamisha cheti cha idhini

**10**.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha cheti cha idhini cha msambazaji baada ya kutokea yafuatayo-

(a) uthibitisho wa msambazaji kujihusisha na vitendo vya kuondoa uaminifu au uongo;
(b) kushindwa kurekebisha VTD isiyofanya kazi ndani ya masaa ishirini na nne, mara tatu mfululizo;
(c) uthibitisho wa kutoa taarifa za uongo au zinazopotosha;
(d) uthibitisho wa kujihusisha na uingiliaji wa utendaji kazi wa VTD;
(e) uthibitisho wa kuwepo kwa udhaifu wa VTD; na
(f) uthibitisho wa ukiukwaji wa kanuni hizi.

(2) Endapo ukiukwaji utahusisha kuvuruga utendaji wa mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa chombo, usajili utasimamishwa kwa muda wa siku zisizopungua thelasini.

(3) Sababu za kusimamisha au kufuta cheti cha idhini zinaweza kutumika kuondoa sifa wakati wa maombi ya kuhuisha cheti cha idhini.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA KUSAMBAZA KIFAA CHA UFUATILIAJI WA MWENENDO WA CHOMBO

Masharti kwa msambazaji wa VTD

**11**.Msambazaji wa VTD atatakiwa-

(a) kusambaza na kufunga VTD kwenye chombo cha mtoa huduma kwa kumuuzia au kumkodisha;

(b) kuwepo kwa huduma za matengenezo ya VTD ilivyosambazwa ndani ya masaa ishirini na nne tangu kutokea au kupata taarifa ya kuharibika VTD;

(c) kuandaa namna ya kuunganisha VTD na mfumo wa VTS kwa kutumia API au kwa njia nyingine iliyokubalika;

(d) kuhakikisha kuwa VTD inatuma taarifa moja kwa moja kwenye VTS;

(e) kuendana na vigezo maalumu vya VTD vitakavyoainishwa na Mamlaka;

(f) kutoa mafunzo ya matumizi ya VTD kwa watoa huduma na wadau wengine;

(g) kuwezesha Mamlaka kuwa na uwezo wa kuingia kwenye VTD pale inapohitajika;

(h) kuhakikisha kuwa taarifa zinazopatika kutokana na huduma anayotoa hazitolewi kwa mtu mwingine bila kupata idhini ya Mamlaka;

(i) kuhakikisha kuwa VTD iko salama na inaunganishwa kwa namna ambayo haitaruhusu kuvurugwa utendaji kazi wake;

(j) kuhakikisha kuwa mafundi wanavaa sare zenye nembo ya msambazaji na kuwa na vitambulisho wanapokuwa kazini;

(k) kuhakikisha kuwa mafundi wanaandaa taarifa ya ukaguzi au matengenezo yaliyofanyika;

(l) kutomsitishia huduma Mtoa huduma bila kutoa taarifa ya awali ya siku thelathini kwa Mamlaka;

(m) kuingia kwenye mkataba na mtoa huduma kabla ya kumuwekea VTD; na

(n) kutoa taarifa kwa Mtoa huduma na Mamlala kuhusiana na hitilafu ya VTD ndani ya masaa sita.

Masharti kwa mtoa

**12**.Mtoa huduma atahakikisha kuwa-

huduma

(a) VTD inayounganishwa katika chombo chake imefungwa na msambazaji aliyeidhinishwa na Mamlaka;
(b) VTD inatunzwa dhidi ya mazingira hatarishi, kuvuruga utendaji kazi wake na kinafanya kazi muda wote;
(c) ikitokea kutokufanya kazi au kuharibika kwa VTD itolewe taarifa ndani ya masaa mawili kwa msambazaji na kama hakuna hatua iliyochukuliwa atoe taarifa kwa Mamlaka ndani ya masaa kumi na mbili tangu ulipotokea uharibifu;
(d) anamruhusu afisa wa Mamlaka au wa msambazaji kufanya ukaguzi wa VTD bila vikwazo;
(e) Mamlaka inapewa taarifa pale ambapo msambazaji hajafanya marekebisho ya VTD ndani ya masaa ishirini na nne; na
(f) analipa malimbikizo ya madeni anayodaiwa na Msambazaji kabla ya kuingia makubaliano na Msambazaji mwingine.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA UJUMLA

VTD isiyoathiri utendaji kazi wa chombo

**13**-(1) Uwekaji wa VTD hautatakiwa kuathiri utendaji kazi wa chombo cha usafirishaji.

(2) Uharibifu wowote utakaosababishwa na ufungaji wa VTD utatakiwa kulipwa na msambazaji.

Gharama za huduma za kadi ya simu

**14**. Msambazaji wa VTD atawajibika kulipia gharama za huduma ya data kutokana na matumizi ya kadi ya simu zinazotolewa na Mamlaka.

Maombi ya upatikanaji wa VTS

**15**.-(1) Mtoa huduma anaweza kuomba kwa Mamlaka upatikanaji wa taarifa za VTS kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa chombo chake.

(2) Endapo Mamlaka itapokea maombi yaliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1), inaweza kumfungulia mtoa huduma akaunti ya ufuatiliaji.

Makosa ya jumla

**16**. Mtu atakayekiuka masharti ya Kanuni hizi atakuwa amefanya kosa na ataadhibiwa kwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki tano lakini isizidi milioni moja au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili.

Mapitio

T.S. Na. 73 la 2020

**17**. Mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Mamlaka chini ya Kanuni hizi anaweza kuomba kufanya mapitio ndani ya siku kumi na nne kutoka siku ya maamuzi, kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu wa Mapitio za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini.

Rufaa

Sura ya 285

**18**. Mtu ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Bodi anaweza kukata rufaa Baraza la Ushindani kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani.

JEDWALI LA KWANZA

*Limetengenezwa chini ya kanuni za 4(1) na 9(1))*

FOMU YA MAOMBI

1. AINA YA MAOMBI / WEKA ALAMA YA PATA KATIKA SANDUKU HUSIKA

| | |
|---|---|
| Mpya | |
| Kuhuisha | |
| Kurudufu | |

2. TAARIFA ZA MUOMBAJI WA CHETI

Jina kamili la Muombaji …………..............................................................
(Jina/Kampuni/Mshirika – kwa HERUFI KUBWA)
Anwani …………………………….......………
Simu ya Ofisi/Simu ya kiganjani: …………………….….
Simu ya kiganjani ya Muombaji: ...………………………..
Barua pepe: …………………………………………………

Anwani ya Makazi:
Mtaa: ……………………………….…….
Namba ya Kitalu: ……………………..…..
Namba ya ofisi: .......................................
Namba ya kitalu ……………………….

Ushawahi kuwa na maombi yaliyokataliwa, kusimamishwa au kufutiwa?

Ndiyo: …...……
Hapana: ………

Kama ndiyo eleza sababu za kukataliwa, kusimamishwa au kufutiwa maombi
………......................................................................………………………………

VITU VYA KUZINGATIA WAKATI WA KUFANYA MAOMBI

1. Maombi ya kwanza yataambatishwa na vifuatavyo:
   (a) nakala ya leseni ya biashara;
   (b) nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi;
   (c) nakala halali ya hati safi ya malipo ya kodi;
   (d) nakala ya kitambulisho cha Taifa au namba kwa mtu binafsi au nakala ya cheti cha usajili wa kampuni

2. Kuhuisha:
(a) uthibitisho wa malipo ya tozo ya mamlaka kwa mwaka ulioisha
(b) nakala ya leseni ya biashara;
(c) nakala ya cheti cha mlipa kodi; na

*Tangazo la Serikali Na.25 (Linaendelea.)*

(d) nakala ya hati miliki ya eneo au mkataba wa pango wa ofisi kama kuna mabadiliko;
(e) nyaraka nyengine yoyote itakayohitajika na mamlaka.

TAMKO

Mimi ninaapa/ninathibitisha/ Sisi tunaapa/tunathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa ni za kweli kwa ufahamu wangu/wetu wote.

Jina Kamili: ………………………………... Sahihi: …………………...

Cheo: ………………………………. Tarehe: ………………………..

ONYO:

1. Ijulikane kuwa kutoa taarifa ya uongo ili kupata cheti kilichoidhinishwa ni makosa ambayo yanaweza kuadhibiwa kwa faini au kifungo.
2. Wasilisha taarifa kwa Mamlaka ikitokea mabadiliko yoyote kwenye taarifa zilizopo kwenye fomu hii, kutokufanya hivyo ni makosa chini ya Kanuni hizi.

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

NAMBA YA JALADA LA MMILIKI

………..........................................

Uhakiki na Idhini

(a) Haijaidhinishwa:

Weka sababu
………………….................................................................................………

(b) Imeidhinishwa:

Tarehe ya kuanza: ……………………….

Tarehe ya kuisha: …………………….......

Jina kamili la Afisa: ……………………………………………………..

Cheo: ……………………………..

Sahihi: …………………………..

Tarehe: ……………………………

Kiasi kilicholipwa: ………………………. Namba ya stakabadhi. ……………………..

Tarehe:...………………………… Sahihi: ……………………….

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(f))*

MAELEZO YA UTEKELEZAJI

| Na. | Maelezo ya Utekelezaji/Ainisho la Kiufundi | Onesha utekelezaji au kutotekeleza | Maoni (ikiwa yapo , Ushahidi au maelezo kuhusu utekelezaji kufikiwa au la) |
|---|---|---|---|
| 1.0 | | | |
| 1.1 | Kutoa na Kufunga VTD wasafirishaji kwa kuwauzia au kuwakodisha. | | |
| 1.2 | kutoa huduma za matengenezo kwa VTD vilivyouzwa au kukodishwa kwa wasafirishaji | | |
| 1.3 | kuandaa kifaa cha kati au utaratibu wa kuunganisha na jukwaa la Mamlaka VTS ukitumia API au utaratibu mwingine uliokubaliwa | | |
| 1.4 | kutekeleza mahitaji yote kama ilivyobainishwa katika API au utaratibu mwingine uliokubaliwa. | | |
| 1.5 | Kuwa na utaratibu/muingiliano utakaowezesha Mamlaka inaweza kuhoji na kudhibiti moja kwa moja kifaa cha kufuatilia kwa wakati halisi na kusasisha baadhi ya vigezo kama vile kikomo cha kasi wakati wowote. | | |
| 1.6 | Hakikisha kwamba data ya GPS inayotumwa kwenye jukwaa la Mamlaka VTS imekamilika na ni sahihi | | |
| 1.7 | kuitaarifu Mamlaka juu ya mabadiliko ya Teknolojia mpya kwenye Mfumo wa Ufuatiliaji na VTD mara kwa mara | | |
| 1.8 | Kuhakikisha kuwa hakuna uvurugaji wa kifaa cha kufuatilia kilichowekwae | | |
| 1.9 | Kuhakikisha VTD zilizofungwa, zinatuma taarifa kwenye VTS saa ishirini na nne – katika siku saba za wiki. | | |
| 1.10 | Kutoa taarifa mara moja kwa Mamlaka kuhusu tukio lolote linaloweza kusababisha VTD kutofanya kazi vizuri (kama vile ajali, wizi n.k.) | | |

*Tangazo la Serikali Na.25 (Linaendelea.)*

| Na. | Maelezo ya Utekelezaji/Ainisho la Kiufundi | Onesha utekelezaji au kutotekeleza | Maoni (ikiwa yapo , Ushahidi au maelezo kuhusu utekelezaji kufikiwa au la) |
|---|---|---|---|
| 1.11 | Kuhakikisha kuzingatiwa kwa viwango vya VTD kama vilivyowekwa na Mamlaka ikiwa ni pamoja na kuunganishwa VTS kwa kutumia API iliyotolewa na Mamlaka | | |
| 1.12 | Kutoa Mafunzo ya VTD zilizofungwa kwa Wasafirishaji na Wadau wengine | | |
| 1.13 | Kutoa nafasi na taarifa kwa Mamlaka wakati wowote kwa ajili ya kupokea data za GPS, ujumuishaji/jukwaa la vifaa vya kati kwa madhumuni ya ukaguzi na uhakikisho wa ubora. | | |
| 1.14 | Kulipa madai ya malipo ya mawasiliano ya GPS/GPRS yaliyotolewa na mteja ndani ya siku saba baada ya wasilisho la madai hayo | | |
| 1.15 | Kutoa alama za GPS | | |
| 1.16 | Kutoa taarifa za tahadhari | | |
| 1.17 | Kusasisha alama za GPS kwa angalau kila dakika 3 | | |
| 1.18 | Kuhifadhi taarifa za tahadhari wakati umetenganishwa na mtandao wa GSM na kusasisha tena hadi seva kuu unapounganishwa kwenye mtandao wa GSM. | | |
| 1.19 | Kutoa tahadhari ya upunguaji wa nguvu za betri | | |
| 1.20 | Vifaa vya ufuatiliaji kutoa tahadhari kuhusu mawasiliano yaliyopotea | | |
| 1.21 | Vifaa vya ufuatiliaji kutoa tahadhari za uharibifu | | |

*Tangazo la Serikali Na.25 (Linaendelea.)*

| Na. | Maelezo ya Utekelezaji/Ainisho la Kiufundi | Onesha utekelezaji au kutotekeleza | Maoni (ikiwa yapo , Ushahidi au maelezo kuhusu utekelezaji kufikiwa au la) |
|---|---|---|---|
| 1.22 | API iliyotolewa au mfumo mwingine wowote wa ujumuishaji uliokubaliwa unaweza kubadilishwa au kusasishwa na Mamlaka kulingana na mahitaji, au mabadiliko ya teknolojia, ambayo yanaweza kusababisha mzabuni kubadilisha jinsi unavyojumuisha au kuwasiliana na VTS pasipo gharama kwa Mamlaka. | | |
| 1.23 | Kuwasilisha nyaraka za vifaa vya kufuatilia (pamoja na itifaki zote zinazohusiana) zinazotumika kwa vifaa visivyo vya BSMART | | |
| 2.0 | | | |
| 2.1 | Nambari ya Usajili wa Chombo | | |
| 2.2 | Jina la Dereva (Kitambulisho cha Dereva kama vile matumizi ya Kitufe cha *i- Button* au mbadala) | | |
| 2.3 | Latitudo (katika desimali) | | |
| 2.4 | Longitudo (katika desimali) | | |
| 2.5 | Mwinuko (kutoka usawa wa bahari) | | |
| 2.6 | Muhuri wa muda wa GPS (MWAKA-MWEZI-SIKU SAA:DK: SEK) | | |
| 2.7 | Mwendokasi (km/h) | | |
| 2.8 | Mwelekeo (Digrii) | | |
| 2.9 | Odomita (KM) | | |
| 2.10 | Idadi ya satelaiti (Nambari inayopokelewa ya satelaiti) | | |
| 2.11 | HDOP (Upunguzaji Mlalo wa Usahihi-Ubora wa mawimbi) | | |
| 2.12 | RSSI (Alama Iliyopokewa ya Nguvu ya Mawimbi) | | |
| 2.13 | LAC (Msimbo wa Eneo la Karibu) | | |
| 2.14 | Utambulisho wa simu | | |
| 2.15 | MCC (Msimbo wa Nchi wa Simu ya Mkononi) | | |
| 2.16 | IMEI (Kitambulisho cha Kimataifa cha Vifaa vya Simu) | | |

*Tangazo la Serikali Na.25 (Linaendelea.)*

| Na. | Maelezo ya Utekelezaji/Ainisho la Kiufundi | Onesha utekelezaji au kutotekeleza | Maoni (ikiwa yapo , Ushahidi au maelezo kuhusu utekelezaji kufikiwa au la) |
|---|---|---|---|
| 2.17 | Muda wa Kupokea Data (Muda Uliopokewa na Seva – MWAKA-MWEZI-SIKU SAA:DK: SEKUNDE) | | |
| 2.18 | Muda wa Mchakato wa Data (Ingiza saa kwenye Hifadhidata - MWAKA-MWEZI-SIKU SAA:DK:SEKUNDE) | | |
| 2.19 | MSG_ID (Data ya kipekee inayoendesha nambari-64bits) | | |
| 3.0 | | | |
| 3.1 | Usogeaji/Kuweka data (Chaguomsingi) | | |
| 3.2 | Kuwashwa Injini | | |
| 3.3 | Kuzimwa Injini | | |
| 3.4 | Mwendo kasi | | |
| 3.5 | Kusimama kwa ghafla | | |
| 3.6 | Kugeuka kwa ghafla | | |
| 3.7 | Kuongeza kasi kwa ghafla | | |
| 3.8 | Kitufe cha dharura (Upande wa Dereva) | | |
| 3.9 | Betri ya Ndani Imepungua | | |
| 3.10 | Betri ya Nje Imechomolewa | | |
| 3.11 | Kuwashwa pasipo kutembea kwa muda mrefu | | |
| 3.12 | Ajali | | |
| 3.13 | Kitufe cha Dharura (Upande wa Abiria) | | |
| 3.14 | Kuvuruga utendaji kazi wa VTD | | |
| 3.15 | Kuweka taarifa kwenye kifaa cha utunzaji taarifa | | |
| 3.16 | Umeme wa Nguvu wa Nje | | |
| 3.17 | Umeme wa Ndani wa Betri ya VTD | | |
| 3.18 | Ripoti ya mafuta | | |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni 4(1), 5(g) na 8(3))*

ADA

| Na. | Aina | Shs. | US $ |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya maombi | 100,000 | 50 |
| 2 | Ada ya cheti cha idhini | 5,000,000 | 5,000 |

Dodoma,
15 Disemba, 2023

MAKAME MNYAA MBARAWA,
*Waziri wa Uchukuzi*